# MKATABA WA UWEZESHAJI KATIKA SHUGHULI YA UCHIMBAJI WA MADINI YA DHAHABU KUPITIA LESENI NDOGO ZA UCHIMBAJI (PMLs)

**KATI YA**

**TANZANIA- ZAMBIA DINGTAI MINING COMPANY LIMITED**

**(MWEZESHAJI)**

**NA**

**MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED**

**(MMILIKI WA LESENI)**


Mkataba huu umeandaliwa na;
Penina Mashimba (Wakili),
Mana and Company Advocates,
Soko la dhahabu mkabala na Nyehunge Pharmacy,
S.L.P 254 - Mwanza.
Simu: 0758 899 151
Barua pepe: peninamashimba254@gmail.com




Penina Mashimba Box 254 Mwanza Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Mkataba huu unatiwa saini Geita leo hii tarehe 31 Mwezi,Disemba 2023 KATI YA **TANZANIA - ZAMBIA DINGTAI MINING COMPANY LIMITED** Kampuni binafsi

Iliyosajiliwa chini Sheria ya Makampuni ya Tanzania (The Companies Act Cap. 212 (RE) 2002) yenye namba za usajiri **170608127**, na yenye Sanduku la Posta **27** Katoro - Geita (itakazojulikana kama **"MWEZESHAJI"** katika mkataba huu) kwa upande mmoja; **NA MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED** Chama cha Ushirika kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Usajiri wa Vyama vya ushirika (Co-operative Society Act R.E 2013) kupitia namba za usajiri **PRI-GT-GEI-TC-2022-623**, chenye makazi yake Mgusu Geita na chenye Sanduku la namba Posta **629** Geita (kitakachojulikana kama **' MMILIKI WA LESENI'**) kwa upande mwingine.

**KWAMBA; MMILIKI WA LESENI** anamiliki kihalali leseni ndogo za uchimbaji wa madini yaani (*Primary Mining Licenses*) **kumi na Sita (16)** zenye namba za usajiri PML**000445LZ, 000444LZ, 000441LZ, 000440LZ, OOO439LZ, 000436LZ, 000449LZ, 000450LZ, 000433LZ, 000434LZ, 000435LZ, 000447LZ, 000432LZ, 00043LZ, 000448LZ** na **000446LZ** zilizopo katika Kijiji cha Mgusu, Wilaya ya Geita Mkoani Geita- Tanzania.

**NA KWAMBA; MMILIKI WA LESENI** kwa hiari yake wenyewe bila kushurutishwa na mtu yeyote yupo tayari kupokea uwezeshaji wa **kiufundi na kifedha** kutoka kwa MWEZESHAJI katika shughuli ya uchimbaji wa madini ya dhahabu kupitia leseni ndogo za uchimbaji wa madini (Primary Mining Licenses) tajwa hapo juu na **MWEZESHAJI** yupo tayari kutoa uwezeshaji huo kwa kuzingatia Sheria ya Madini ya Tanzania (The Mining Act Cap 123).

**IZINGATIWE KUWA**; Pande zote mbili zinauwezo kisheria wa kufunga mkataba na zimekubaliana kuingia katika mkataba huu kwa hiari yao na kwa masharti yaliyoelezwa ndani ya mkataba huu;

**HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YA KWAMBA;**

**1. DHUMUNI LA MKATABA**

Dhumuni kubwa la Mkataba huu ni MWEZESHAJI kumuwezesha MMILIKI WA LESENI katika shughuli za uchimbaji wa madini ya dhahabu kupitia leseni ndogo za uchimbaji wa madini yaani (*Primary Mining Licenses*) **kumi na Sita (16)** zenye namba za usajiri PML**000445LZ, 000444LZ, 000441LZ, 000440LZ, OOO439LZ, 000436LZ, 000449LZ, 000450LZ, 000433LZ, 000434LZ, 000435LZ, 000447LZ, 000432LZ, 00043LZ, 000448LZ** na **000446LZ**. Mradi huo wa uchimbaji wa madini ya dhahabu unatarajia

kufanyika katika Kijiji cha Mgusu, Wilaya ya Geita Mkoani Geita-Tanzania.

2. **MCHANGO NA MAJUKUMU YA PANDE ZOTE MBILI KATIKA MRADI**

**Mchango wa Mwezeshaji :**

i.) MWEZESHAJI atatoa kiasi cha Dola za Kimarekani **Milioni 23.5** kama mtaji wa kuwezesha shughuli za uchimbaji na uchakataji wa zahabu katika eneo hilo la uchimbaji lenye leseni tajwa hapo juu.

ii.) MWEZESHAJI atatakiwa kutoa kiasi cha shilingi milioni mia tano ( TZS 500,000,000/=)

kama ada ya kusaini kusaini mkataba (signing allowances) kwa Mmiliki wa leseni kiasi ambacho kitatoka mara baada ya kusaini mkataba huu, pesa hii haitarudishwa , na ndio itatumika kujikimu kwa mmiliki wa leseni katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.

**A. Majukumu ya Mwezeshaji:**

**MWEZESHAJI atakuwa na majukumu yafuatayo katika kuwezesha mradi huo wa uchimbaji wa dhahabu-;**

i. Kuhakikisha shughuli za uchimbaji wa dhahabu Zinaanza mapema baaada ya kusaini mkataba huu kwa kutoa fedha ya uendeshaji wa shughulu hiyo bila kuchelewa wala kukosa.

ii. Kuwajibika katika taratibu za uchimbaji na uchakataji wa dhahabu kwa kuweka vifaa vyote husika vya uchimbaji vinavyotakiwa ikiwa ni pamoja na wafanyakazi (wenye utaalamu na vibarua).

iii. Kutoa ulinzi wa mali zake mwenyewe na kuhakikisha usalama wa mazingira ya mahali pa kazi ,kujali Afya za wafanyakazi wake, kwa mujibu wa sharia za mazingira.

iv. Kulinda na kuhifadhi miondombinu ya mazingira ikiwa ni pamoja kuepusha uchafuzi wa mazingira usiofaa,kulinda na kutunza uoto wa asili katia maeneo asiyoyafanyia kazi lakini yanamilikiwa na mmiliki wa leseni hizi tajwa.

v. Kutoa haki kwa MMILIKI WA LESENI au WAKALA wake anayetambulka kisheria Kuingia

vi. na kukagua mwenendo wa shughuli za uchimbaji unaofanyika,kwa wakati wowote atakaoona unafaa ili kujua mwenendo wa kazi zao, hapatakuwa na maeneo ambayo mmiliki wa leseni hatakiwi kuingia kwa sababu yeyote ile .

Penina Mashimba Box 254 Mwanza Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

**Mwezeshaji atatekeleza vitu vifuatavyo kwa jamii katika mradi huo:-**

a. Kutoa nafasi za ajira kwa wakazi wa Kijiji cha Mgusu na maeneo yanayozunguka mgodi huo wa dhahabu ambao wanakidhi vigezo vya kuajiriwa au wenye uwezo wa kufanya kazi.

   Kwamba, katika kutoa nafasi hizo za ajira, **MWEZESHAJI** atawapa kipaumbele wanachama wa Chama cha Ushirika cha Mgusu Miners Co-operative Socirty Limited.

b. Kuhusika na kujitoa/ kuwajibika kwa jamii (Co-operate Social Responsibility) kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya kunufaisha jamii kwa ujumla inayozunguka eneo la mgodi.

c. Kujenga shule moja ya msingi katika eneo ambalo mwekezaji ataelekezwa na uongozi husika.

d. Kuwajibika na ulipaji wa fidia halali kwa wananchi ambao watalazimika kuondoka ili kupisha shughuli hizo za uchimbaji wa dhahabu, ulipaji huu ni lazima upitie kwa mmiliki wa leseni kwani kimsingi yeye ndio anejua kiwango cha fidia kinachokizi .

**Mchango wa Mmiliki wa Leseni :**

MMILIKI WA LESENI atatoa eneo la uchimbaji katika leseni zake ndogo za uchimbaji madini **kumi na Sita (16)** zenye namba za usajiri **PML000445LZ, 000444LZ, 000441LZ, 000440LZ, OOO439LZ, 000436LZ, 000449LZ, 000450LZ, 000433LZ, 000434LZ, 000435LZ, 000447LZ, 000432LZ, 00043LZ, 000448LZ** na **000446LZ** zilizosajiliwa kwa jina la **MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED** lililopo katika kijiji cha Mgugu Wilayani Geita na Mkoani GeitaTanzania.

**Majukumu ya Mmiliki wa Leseni:**

**MMILIKI WA LESENI atakuwa na majukumu yafuatayo katika kuwezesha mradi huo wa uchimbaji wa dhahabu-;**

a) Kusimamia ulinzi wa eneo linalozunguka mgodi ikiwa ni pamoja na ulinzi kwa MWEZESHAJI.

b) Kutotumia pesa ya mradi wa uchimbaji wa dhahabu kwa matumizi mengine tofauti na matumizi yaliyokusudiwa katika mradi.

c) Kutoruhusu mtu mwingine afanye shughuli za uchimbaji katika eneo la mradi lenye leseni husika tajwa hapo juu.

Penina Mashimba
Box 254 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

d) Kutoingia katika mkataba na mtu au kampuni yoyote wa uchimbaji wa dhahabu kuhusiana na leseni tajwa hapo juu bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa MWEZESHAJI katika kipindi cha mkataba.

e) Kufuata sheria na taratibu sahihi zinazohusiana na umilki wa leseni.

f) Kufuata taratibu sahihi za Sheria ya madini (the Mining Act, Cap 123) ikiwa ni pamoja na kuhuisha leseni za uchimbaji tajwa hapo juu ndani ya muda bila kuchelewa.

**3. MAJUKUMU YA PAMOJA**

Kwamba kutakuwa na majukumu ya pamoja ambayo yatafanyika kwa pamoja na kwa ushirikiano baina ya MMLIKI WA LESENI na MWEZESHAJI katika kuendesha shughuli zao za uchimbaji wa dhahabu:-

a. Kusimamia zoezi la mwisho la uchomaji na wa MALI (dhahabu) katika hatua ya mwisho ya uchenjuaji ili kufanya pande zote kujiridhisha juu ya kiasi cha dhabu kilichopatikana.

b. Kusimamia zoezi la uuzwaji wa dhahabu katika ofisi husika ya ununuzi wa dhahabu kwa kuzingatia bei sahihi iliyopo sokoni siku hiyo.

c. Kusimamia mgao wa wa hisa zao kwa mujibu wa makubaliano yaliyomo ndani ya mkataba.

d. Kuhakikisha kodi zote za serikali zinalipwa kwa wakati kama vile(mrahaba ,service revy,withholding tax n.k) kabla ya mgao kufanyika.

e. KWAMBA ni lazima Kusimamia ulinzi na usalama wa mali zao, kuzuia na kudhibiti utoroshaji wa dhahabu ,kulinda Afya za wafanyakazi,pamoja na kutetea uoto wa asili wakati wote wa utekelezaji wa mkataba huu,ikiwa ni pamoja na kutunza na kulinda vyanzo vya maji.

f. KWAMBA Kuwepo kwa vikao vya pamoja ili kujadili mwenendo wa kazi yao, pamoja na kutunza kumbukumbu za vikao vyao na uzalishaji utakaokuw umepatikana ili kjipa nafasi ya kufanya tathimini ya mwenendo wa kazi yao.

g. KWAMBA wanakubaliana kuwa watakuwa na njia sahihi ya mawasiliano katika kusimamia shughuli zote za uchimbajiwa wa madini ya zahabu kwa kipindi chote cha mkataba.

h. KWAMBA, MWEZESHAJI na MMILIKI WA LESENI kwa pamoja watasimamia zoezi la uchimbaji na uzalishaji wa dhahabu katika mradi huo

i. KWAMBA pande zote mbili zinakubaliana kuwa watafanya uchimbaji wao bila kuingilia maeneo ambayo tayali yanachimbwa

Penina Mashimba
Box 254 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

na wachimbaji wadogo ambao tayali wapo katika leseni hizi na hivyo kwaacha huru katika maduara yao.

4. **MGAWANYO WA FAIDA**

MWEZESHAJI na MMILIKI WA LESENI wanakubaliana kuwa baada ya zoezi zima la uchimbaji na uzalishaji wa dhahabu kukamilika, watatoa malipo yote ya Serikali ambayo ni ada ya mrahaba (royality),ukaguzi, TRA na ushuru wa huduma (Service Levy) na kisha fedha itakayobaki itagawanywa katika asilimia 85% kwa MWEKEZAJI na 15% kwa mmliki wa leseni kama inavyoanishwa kwenye jedwali lifuatalo:-

| NO | JINA | IDADI YA HISA(%) | SAHIHI |
|---|---|---|---|
| 01 | TANZANIA - ZAMBIA DINGTAI MINING COMPANY LIMITED | 85% | YAN JIAN YUN<br>xiong fei yue |
| 02 | MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED | 15% | |

TANZANIA-ZAMBIA DINGTAI MINING CO. LTD
31 DEC 2023
P.O. BOX 27
GEITA

MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY
PRI-GT-GEI-TC
2022-623
TAR 30/12/2023
S.L.P 629 GEITA

**5. VIFAA NA MASHINE ZA MRADI WA UCHIMBAJI DHAHABU**

MWEZESHAJI na MMILIKI WA LESENI wanakubaliana kuwa vifaa vyote na mashine vitakavyowekwa na MWEZESHAJI katika mradi huo vitabaki kuwa mali ya Mwezeshaji mkataba huu utakapofika mwisho, isipokuwa vifaa vya kawaida kama majembe, fyekeo na vitu vilivyojengwa vya kudumu kama nyumba au fensi zitabaki kuwa mali ya mmiliki wa leseni.

**6. MUDA WA MKATABA**

a. MWEZESHAJI na MMILIKI WA LESENI wanakubaliana kuwa mkataba huu utakuwa ni wa muda wa miaka **mitano (5)** kuanzia tarehe ya kusaini mkataba huu. Na kwamba baada ya kipindi cha miaka mitano kuisha, pande zote mbili zitakaa chini na kujadiri mashariti ya mkataba upya kabla ya kusaini.

b. Kutakuwa na nafasi ya kubadadili kwa ama kupunguza au kuuongeza baadhi ya vifungu ambavyo pande zote zitaona vifanaa ndani muda wa utekelzaji wa mkataba huu.

7. A. **UKOMO WA MKATABA**

Mkataba huu utakoma bila madhala yeyote mara baada ya mambo haya kutokea;-

i). kufika kikomo chake kwa mujibu wa kifungu cha **6** cha mkataba huu.

Penina Mashimba
Box 254 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

(ii). MWEZESHAJI kushindwa kulipa kwa wakati ADA ya kusaini mkataba yaani (signing allowance) kama ilivyo anishwa katika kifungu cha 2(ii) cha mkataba huu.

iii) Upande mmoja kutoa notisi ya mannishi ya kutokuwa na nia ya kuendelea na mkataba huu kwa kipindi kisichopungua miaka 2 kabla ya kusitisha mkataba.

iv). Kutokea kwa madhara yaliliyo nje ya uwezo wao **(FORCE MAJEURE)** kama vile milipuko,mafuliko,vita,au maandamano, machafuko ya kisiasa au nchi kuingia kwenye hali ya hatari n.k ambayoyatatokea katika kipindi cha utekelezaji wa mkataba huu.

**B. Mkataba huu utakoma kwa madhala endapo haya yatatokea:-**

**i). MWEZESHAJI kushindwa kuanza utekelezaji wa mkataba huu kwa kipindi cha miezi 6 baada ya kusaini makubaliano haya bila sababu yeyote ya msingi wala bila kutoa taarifa yeyote ya maandishi basi atakuwa amevunja mkataba atatakiwa kilipa faini ya shilingi milioni mia mbili (Tsh 200,000,000/=) kama fidia ya ukiukwaji wa mashariti ya mkataba huu.**

**ii). KWAMBA endapo Upande wowote utashindwa kutekeleza mashariti ya mkataba huu ikiwa ni pamoja na kuvunja mkataba huu bila notisi yeyote ile, basi upande huo utalazimika kuufidia upande ulioathilika juu ya madhala ya uvunjwaji wamkataba huu .**

**8. UTATUZI WA MIGOGORO**

Mkataba huu utaongozwa na kutafasiriwa kwa kufuata sheria za Tanzania. Na kwamba endapo utatokea mgogoro wowote kuhusiana na mkataba huu basi mgogoro huo utajadiliwa kwa njia ya Amani na endapo itashindikana sheria za madini na za mikataba za Tanzania zitatumika katika kutatua mgogoro huo ikiwa ni pamoja na Mahakam yenye uwezo wa kutatua mgogoro huo. (Competent Court).

**HIVYO BASI** kwa **pande zote mbili** kutia saini zao hapa chini kwa tarehe, mwezi na mwaka tajwa hapo mwanzo wanakiri na kukubali kuheshimu na kufuata masharti yaliyoelezwa ndani ya mkataba huu.

Umetiwa saini na kutolewa Geita na **TANZANIA - ZAMBIA DINGTAI MINING COMPANY LIMITED** leo hii tarehe ...31..... mwezi ...12...... 2023.

Jina: ...YAN JIANYUN...
Saini: ...[signature]...
Anuani: ...P.O BOX 27 KATORO -GEITA...
Wadhifa: ...MKURUGENZI...
Tarehe:...31/12/2023...

TANZANIA - ZAMBIA DINGTAI MINING CO LTD
31 DEC 2023
P.O. BOX 27
GEITA

Penina Mashimba
Box 254 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Jina: Xiong fei Yue
Saini: Xiong fei Yue
Anuani: P.O BOX 27 KATORO - GEITA
Wadhifa: Mkurugenzi
Tarehe: 31/12/2023

TANZANIA-ZAMBIA DINGTAI MINING CO. LTD
31 DEC 2023
P.O. BOX 27
GEITA

MBELE YANGU (WAKILI)
Jina: PENINA MASHIMBA
Saini: ...
Anuani: BOX 254 MWANZA
TAREHE 31/12/2023

Penina Mashimba
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths

Umetiwa saini na kutolewa Geita na **MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY**
**LIMITED** leo hii tarehe 31 mwezi 12 2023

Jina: MASATILE MODEST
Saini: ...
Anuani: S.L.P 629
Wadhifa: MWENYEKITI
Tarehe: 31/12/2023

MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY
PRI-GT-GEI-TC 2022-623
TAR 31/12/2023
S.L.P 629 GEITA

Jina: ZACHARIA NHUMA ICARALA
Saini: ...
Anuani: S.L.P 629 - GEITA
Wadhifa: KATIBU
Tarehe: 31-12-2023

KATIBU MKUU
MGUSU MINERS CO-OPERATIVE SOCIETY LTD
PRI-GT-GEI-TC-2022-623
GEITA.

Jina: ERICK JOSEPH KAROLA
Saini: ...
Anuani: 629
Wadhifa: MWAKILISHI WA WANACHAMA
Tarehe: 31/12/2023

MBELE YANGU (WAKILI)
Jina: PENINA MASHIMBA
Saini: ...
Anuani: BOX 254 - MWANZA
Tarehe: 31/12/2023

Penina Mashimba
Box 254 Mwanza
Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths